IDARA YA HUDUMA ZA UBORA WA BIDHAA

1.0. Utangulizi

Idara ya Huduma za Ubora wa Bidhaa ina vitengo vitatu ambavyo ni Chakula na Dawa, Mikrobioloji na Huduma ya mitambo.

2.0. Majukumu ya Idara

- Kufanya uchunguzi wa kitaalamu wa sampuli za vyakula, vinywaji na dawa kwa kutumia viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Kufanya uchunguzi wa mikrobiolojia ya vyakula, vinywaji, dawa na mazao yake.
- Kutoa mafunzo mbalimbali na ushauri wa kisayansi kwenye taasisi na jamii kwa ujumla.
- Kufanya tafiti mbalimbali za kisayansi na kutoa ushauri kwa wadau.
- Kutoa ushahidi mahakamani.

3.0. Wateja Wetu

- Wizara, Idara na Wakala mbalimbali,
- Polisi na Mahakama,
- Mashirika ya Umma,
- Bodi za Kitaaluma,
- Vyuo mbalimbali na Taasisi za Utafiti,
- Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mashirika ya Dini,
- Mashirika ya Kimataifa,
- Wafanyabiasha na Wajasirimali,
- Viwanda.

4.0. Bidhaa Zinazofanyiwa Uchunguzi

- Vinywaji vikali (Konyagi, viroba, wiski, vodka, gin n.k),

- Pombe za viwandani na kienyeji (Bia, mvinyo, pombe za nafaka na gongo),

- Sukari, asali, chai, kahawa, kokoa na viungo,
- Vinywaji baridi (maji, soda, juisi n.k),
- Maziwa na mazao yake,
- Nafaka na mazao yake,
- Mafuta ya kula,

- Matunda na mboga pamoja na mazao yake,

- Nyama na Samaki pamoja mazao yake,
- Dawa za binadamu na dawa asilia,
- Dawa za mifugo, wadudu na mimea,

5.0. Faida za Kutumia Huduma Zetu

- Kulinda afya za binadamu, wanyama na mazingira,
- Kuongeza kipato kwa jamii, taasisi na taifa kwa ujumla,
- Kulinda nchi isiwe jalala la bidhaa hafifu na zilizopita muda wake.

6.0. Hasara za Bidhaa zisizo na Ubora

- Bidhaa hafifu na zisizo na ubora zinaweza kusababisha madhara mbalimbali ya kiafya kama vile: kuhara, maumivu ya tumbo, kichwa, kansa na hata kifo.
- Dawa hafifu na zisizo zisizojulikana ubora zinaweza kusababisha mwili kupungua nguvu za kujikinga na maradhi na hata kifo.
- Kwa upande wa vyakula zinaweza kusababisha utapia mlo na kwashakoo.

7.0. Watendaji katika Idara

Idara ina wafanyakazi wenye ujuzi waliobobea katika taaluma za fani ya kemia, vyakula, dawa, lishe, mikrobiolojia na uendeshaji wa mitambo ya maabara.

8.0. Programu za Uchunguzi na Ithibati

- Maabara imekuwa ikishiriki kwenye mashindano ya Kitaifa na Kimataifa (PT) kufanya uchunguzi wa bidhaa mbalimbali za vyakula, mikrobiolojia na dawa ili kujipima ubora wa huduma za kimaabara tulionao katika kukidhi vigezo vya Kitaifa na Kimataifa.
- Wakala kwa sasa imepata vyeti vinavyotambulika Kimataifa vya uendeshaji bora wa maabara ambavyo ni ISO 9001:2008 na ISO 17025:2005.

9.0. Aina za Uchunguzi wa Kimaabara zinazofanyika

Baadhi ya chunguzi za kimaabara ni: kiwango cha kilevi na sumu (methanol) kwenye pombe, vyakula, vinywaji, utungaji (food composition), madini, dawa za wadudu, mikrobiolojia (*coliforms, salmonella, staphylococcus, yeast*, *mycotoxins)* ubora wa dawa za binadamu, mifugo na dawa asilia.

10.0. Vifaa vya Kisasa vya Maabara

Idara ina vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa kimaabara. Baadhi yake ni:

- **Automatic Kjeldahl** kwa ajili ya kupima protini kwenye vyakula na mashudu.
- **Fourier transform infrared spectroscopy (FTIR)** inatumika kuchunguza dawa za kulevya, damu, dawa za binadamu, mifugo, wadudu na mimea n.k.
- **High Performance Liquid Chromatography (HPLC)** hutumika kuchunguza; kiwango cha kilevi na sumu (methanol) kwenye pombe, vitamini, dawa, damu na dawa asilia n.k.
- **Induced Couple Plasma Optical Emission Spectrometer (ICP-OES)** inatumika kupima madini mbalimbali, udongo, kemikali n.k.
- **Gas Chromatography Mass spectrometer** (GCMS/MS) hutumika kuchunguza dawa za wadudu na mimie, dawa za binadamu n.k.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Mkemia Mkuu wa Serikali
Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali
Luthuli/ Barack Obama Drive
S.L.P. 164
Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: + 255 22 2113383/4
Nukushi: +255 22 2113320
Baruapepe: cgc@gcla.go.tz, gcla@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Mashariki
Luthuli/Barack Obama Drive
S.L.P. 164
Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: + 255 22 2113383/4
Nukushi: +255 22 2113320
Baruapepe: gcla.east@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Ziwa,
Eneo la Hospitali ya Sekou Toure/Isamilo
S.L.P. 502,
Mwanza, Tanzania.
Simu: +255 28 2500279
Baruapepe: gcla.lake@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Kaskazini
Kituo cha Afya Themi
S.L.P. 2095
Arusha, Tanzania.
Simu: +255 27 2506394
Nukushi: +255 27 2549026
Baruapepe: gcla.north@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
Eneo la Hospitali ya Mkoa wa Mbeya
New Forest Area
S.L.P. 2875
Mbeya ,Tanzania.
Simu: +255 25 2502311
Nukushi: +25525 250 312
Barua pepe: gcla.southern@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Kusini
Ushirika House
Barabara ya TANU
S.L.P. 1414
Mtwara,Tanzania.
Simu: +255 23 233 4760
Nukushi: +255 23 233 4761
Barua pepe: gcla.south@gcla.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

ISO 9001:2008
ISO 17025:2005

IDARA YA HUDUMA ZA UBORA WA BIDHAA